

Uwe Tayari kwa Canvas!



Ili kusambaza kwa mafanikio jukwaa la Canvas la Shule za Umma za Kaunti ya Fayette za shule za kati na za secondary, tumeunda hati hii ili kusaidia wanafunzi na familia kuwa watendaji katika kuhakikisha kwamba vifaa vyao vimetayarishwa. Tafadhali fuata hatua zifuatazo ili kuandaa Canvas **KABLA** ya siku ya kwanza ya mwaka wa shule 2020-21.

1. Futa Kashe ya Kivinjari (Browser).
2. Zima vifaa na Anzisha tena.
3. Sasisha kivinjari cha Chrome cha vifaa visivyo vya Chromebook.
4. Ruhusu kuki zote.
5. Ingia kwenye Canvas.
6. Wasiliana na Dawati la Msaada wa Wanafunzi / Familia kwa msaada, 859-381-4410.

1. Futa Kashe ya Kivinjari

Vivinjari (browsers) vyote vinafaidika na kusafisha kashe, lakini kivinjari cha Chrome kinajibu vizuri zaidi wakati kinasafishwa mara kwa mara. Mtumiaji anaweza kutoka kwa akaunti ya kibinafsi ya Gmail, lakini mara nyingi kashe hudumu nyuma ya pazia. Hali hii mwishowe inaweza kuleta migogoro na barua pepe ya FCPS, na Canvas vivyo hivyo.

- Hatua za kufuta Kashe ya Kivinjari [“Steps to Clear Browser Cache”](#) (Lugha nane zinazotolewa)

2. Kuzima Vifaa

Wakati vifaa havizimishwe na kuwashwa tena mara kwa mara, vinaweza kusababisha matatizo kwa Canvas na majukwaa mengine mengi ya mkondoni. Chromebooks haswa zinapatwa na matatizo mengi. Fahamu pia kwamba kufunga skrini sio sawa na kuzima na tena kuwasha kifaa. Ofisi ya Teknolojia ya Ufundi ya FCPS inapendekeza kutumia “Power button” (“kitufe cha umeme”) kwa kuzima vifaa mara moja kwa wiki.

3. Sasisha Kivinjari cha Chromebook

Kwa kifaa chochote kisicho cha Chromebook, hakikisha kusasisha Kivinjari cha Chrome kwa "Version 83" ("Toleo la 83"). Kivinjari kilicho kwenye Chromebook kinapaswa kusasishwa wakati kifaa kinazimwa na kuwashwa, kama ilivyotajwa kwa # 2 hapo juu.

4. Ruhusu kuki zote

Mara tu ukimaliza Hatua 1 na 2, hakikisha unaingia katika kivinjari, haswa Chrome, na uwezeshe Mpangilio wa "Allow all cookies" ("Ruhusu kuki zote").

- Fungua Mipangilio ya Chrome kwenye kona ya juu ya kulia ya skrini.
- Bonyeza kwa faragha (privacy) na usalama (security) vilioko kwenye pipa (sidebar) la kushoto.
- Chagua kuki na data za tovuti ingine.
- Angalia, Ruhusu kuki zote.

5. Ingia kwenye Canvas

Ili kugundua maswala yoyote ya kuingia mbeleni, tafadhali ingia kwenye Canvas kupitia programu ya "Google Drive App" kabla ya Agosti 26, 2020. Utaratibu ni ule ule kama kwa Darasa la Google, EnVision, Collections, na majukwaa mengine ya mtaala. Sogeza chini tu ndani ya waffle ili upata chapa ya Canvas na ubonyeze kwa kufungua.

Tafadhali pigia simu **Dawati la Msaada wa Teknolojia kwa Familia** kwa usaidizi ku nambari 859-381-4410 ikiwa haukufanyikiwa kuingia kwenye Canvas.

- Mwongozo wa Canvas kwa Wanafunzi [Canvas Guide for Students](#) - ina picha ya Programu ya Hifadhi ya Google (Google Drive Apple waffle).
- Mwongozo wa Canvas kwa Familia [Canvas Guide for Families](#)

(Bonyeza hapa "[Click for additional language translations](#)" kwa tafsiri ya lugha ya miongozo yote miwili.)

Picha inayofuata inaonyesha jinsi Dashibodi ya Canvas ya kawaida inafanana ukifanyikiwa kuingia.

The screenshot shows the Canvas dashboard interface. On the left is a blue sidebar with navigation options: Account, Dashboard, Courses, Calendar, Inbox, and Help. The main content area displays a 'Nothing More To Do' message with a 'Scroll up to see your history!' prompt and an 'Add To-Do' button. Three green-bordered text boxes with arrows pointing to specific elements provide instructions in Swahili:

- Top-left box:** Ikiwa unaweza kuona skrini hii na urambazaji wa rangi ya bluu, umeingia KIKAMILIFU kwenye Canvas. (If you can see this screen and the blue color, you have successfully logged in to Canvas.)
- Top-right box:** Ballon ni nini Daschboards ya wanafunzi wengi itaonekana kama walimu wao KUPUNGUA kozi yao. Wanafunzi wengine wanaweza kuona kozi za zamani. (Balloons are what many students' dashboards will look like as their teachers' classes drop. Other students may see old classes.)
- Bottom-right box:** Dashibodi zingine zinaweza kuonyesha mwonekano wa orodha, badala yake, na picha ya "televisheni" juu ya skrini. Chini ya picha hiyo itakuwa kifungu, Mwanzo wa Historia yako ya Kufanya. (Other dashboards may show a list view, instead of the "television" picture on the screen. Below that picture will be a button, Start of your History.)

At the bottom of the dashboard, the 'INSTRUCTURE' logo is on the left, and 'Privacy Policy', 'Acceptable Use Policy', 'Facebook', and 'Twitter' links are on the right.

6. Wasiliana na Dawati ya Msaada wa Wanafunzi / Familia kwa msaada, 859-381-4410

Ikiwa haukufaulu kuingia kwenye Canvas, tafadhali wasiliana na Dawati ya Msaada kwa usaidizi. Wanaweza kusaidia na kuweka nenosiri mpya au kuhusu maswala mengine ambayo yanaweza kuzuwiya uingiaji kwenye Canvas.



Fayette County Public Schools

Office of
Instructional
Technology